
Jarida la kanisa jipya la kimitume afrika mashariki

Toleo la 2, Juni, 2012

# African Joy

*Toleo la bure*



- **Ujumbe kutoka kwa Mtume Mkuu**
- **Habari za kikanda**

**Ibada Takatifu**
**Mtume Mkuu akiwa**
# Tanzania





# Mtume Mkuu akiwa Tanzania

Mwishoni mwa juma la tarehe 12-14 Agosti 2011 Mtume Mkuu Leber alitembelea nchi ya kiafrika ya Tanzania. Ibada mbili takatifu ziliratibiwa hapa, moja ikiwa siku ya Jumamosi huko Mbeya na nyingine siku ya Jumapili, Ibada ya mwisho huko Mwanza, Mtume Mkuu alimstaafisha Mtume Nzarombi na D. Seulu, pamoja na askofu N. Bejumula na kuwatakia mapumziko mema. Kisha akawaweka wakfu mitume saba na maaskofu watano kwa ajili ya kuhudumia Makanisa ya Kiwilaya.

Wapendwa wangu sana akina kaka na dada, Maneno yaliyopo kwenye somo yalitolewa kwa wana wa Israeli. Hawakufika Jerusalem kabisa na walitaka kurudi nyuma. Mungu akawapatia Unabii huu. Akasema kwamba wangeimiliki nchi na kuurithi mlima Mtakatifu, lakini kulikuwa na hitaji moja tu: walipaswa kumwamini Yeye. Hili bado linakubalika leo hii tunapigania utukufu. Tunapigania utukufu wa milele, bali tunapaswa kufanya jambo moja. Lazima tuweke imani yetu kwa Mungu.

Kumwamini Mungu kuna vipengele vingi. Tunaposema tunamwamini Mungu, kisha tunaliamini na neno lake. Ibrahimu aliamini neno la Mungu. Siku moja Mungu akamwambia, Ondoka kwenye nchi yako, acha kila kitu nyuma; nenda kwenye nchi nitakayokuonyesha. Ibrahamu akafanya hivyo. Na tuweke imani yetu katika yale tunayoyasikia kwenye ibada takatifu kwa maana hilo ndilo neno la Mungu.

Ninamfikiria Petro aliyejaribu kuvua samaki usiku kucha, lakini hakupata kitu. Bwana akamwambia: Nenda tena katupe jarife (nyavu) zako upande mwingine. Petro akafanya hivyo,





"... Lakini yeye anayenitumaini ataimiliki nchi na kuurithi mlima wangu Mtakatifu."

— *Isaya 57, sehemu ya aya ya 13*

kwa sababu alilielewa neno la Mungu, akasema; hakupata samaki hata mmoja usiku kucha, kwa sababu ya neno lako, nitafanya hivyo, amini neno la Mungu.

Kuna mfano mwingine wa Petro katika hali ya tofauti sana. Alikuwa pamoja na wanafunzi ziwani. Bwana Yesu hakuwa pamoja nao, Lakini ghafla akawatokea juu ya maji. Petro akasema: Bwana kama wewe ndiye, niamuru nije kwako juu ya maji (Mathayo 14:28) Bwana Yesu akasema: njoo! Na kwa kweli Petro alitoka kwenye mtumbwi na aliweza kutembea juu ya maji. Kisha akaona mawimbi, aliogopa na akaanza kuzama. Kwa hiyo hapo kuna jambo fulani tunaliweza kujifunza: Lazima kuweka imani yetu yote kwa Mungu.

Pia tuweke imani yetu katika kuongozwa na Bwana. Wakati mwingine kunakuwa na hali ngumu na matatizo. Bali tuwe na imani kwamba Mungu wetu anafahamu kinachoendelea. Atatuongoza kwenye magumu haya iwapo tunaweka imani yetu kwa uongozi Wake!

Na tuweke imani yetu kwenye baraka za Bwana, kwa sababu tunatambua kwamba Baba yetu wa mbinguni anaweza kutubariki zaidi ya ufahamu wetu. Tunapotaka kubarikiwa, kisha na tumtolee yeye sadaka zetu na kumtumikia Yeye.

Acha nitaje kipengele cha mwisho: Na tuweke imani yetu katika ahadi alizozitoa Mungu. Tunafahamu kwamba Bwana Yesu aliahidi kuja tena na atatimiza ahadi hiyo. Hatujui ni lini. Inaweza kuwa hata leo.

Kwa hiyo tunaona kwamba kuweka imani yetu kwake kuna vipengele mbali mbali. Na tuweke imani yetu kwenye neno lake, uongozi wake, baraka zake, na tuweke imani yetu katika ahadi aliyoitoa. Kisha tutakubalika siku atakapokuja Bwana Yesu na tutaungana pamoja naye milele yote. *(Imefupishwa)*





N E N O   L A   S A L A M U

# Pentecoste ya Mwaka 2012

Imekwishakuwa ni tabia yenye heri kuwa na neno la salamu ya Kipentekoste kwa watu wa Mungu duniani kote. Niliomba kwa ajili ya neno maalum na ilikuwa ni furaha kulipokea neno hili lifuatalo la "Bali akasema, 'Mambo yasiyowezekana kwa wanadamu, yanawezekana kwa Mungu." Leo hii mara kwa mara tunaona jinsi tunavyofikia kikomo chetu upesi. Jinsi ilivyo vyema kufahamu kuwa kwa Bwana hakuna ukomo. Katika neno hili linasema kwamba kwa Mungu mambo yote yanawezekana kisha ninataka niseme: "Kwa Mungu mambo yote yanawezekana." Tunapoutumia uweza wake wote kisha tunaweza kufanikisha mambo ya kibinadamu ambayo vinginevyo tusingeweza kufanikisha. Katika hili nisingependa kuelekeza macho yetu kwenye miujiza ya kidunia. Ningependa kuzungumzia zaidi kuhusu mambo ya kiroho ambapo neno hili linaweza kuwa kwa ajili yetu hasa. Acha nitaje mambo machache.

✤ Pengine kuna ghadhabu na kutokuelewana kati ya watu na hawawezi kufikia kukubaliana kabisa. Hali kama hiyo inaweza ikaendelea kwa majuma kadhaa na pengine hata miezi. Kwa binadamu itaonekana kwamba haiwezekani kukawa na mapatano, bali kwa Mungu hiyo inawezekana.

✤ Jambo lingine inaweza kuwa familia imetengana wanafamilia wote wameendeleza utengano kati yao. Kwa wakati huo inaonekana kama hakuna jinsi ya kurejea hali yao ya kwanza. Kwa mwanadamu hili haliwezekani, bali kwa Mungu linawezekana.

✤ Sisi wote tuna tabia zetu binafsi na wakati mwingine si tabia njema. Kwa hakika tunapenda kurekebisha tabia hizi mbaya na kisha tunaona kwamba siyo rahisi sana kurekebisha. Mara kwa mara tunaanguka kutenda mambo ambayo si sahihi. Kwa binadamu inaonekana kwamba haiwezekani kurekebisha tabia mbaya ya mtu, bali kwa Mungu inawezekana.

✤ Ninataka kwenda mbali kidogo na kulielezea neno hili katika hali ya kidunia ambayo ndani yake tunaishi, sisi wenyewe. Tunajua kwamba Ukristo ni kujifunza upya. Na iwapo tungetazama siku za usoni pia tunaweza kuogopa kidogo. Swali laweza kutokea:- Ni jinsi gani mambo yatakavyosonga mbele? Iwapo tunatazama kwenye makusanyiko yetu yenyewe nako pia kuna mashaka na matatizo yanayotufanya tushangae ni jinsi gani tutasonga mbele katika siku za usoni: kutazama mambo haya katika hali ya kibinadamu yanakuwa magumu sana kwetu. Bali kwa Mungu kila kitu kinawezekana. Pia Mungu anaweza kuyabadili matatizo ya wakati wetu maana kwake hakuna lisilowezekana.

> "Yasiyowezekana kwa wanadamu yawezekana kwa Mungu."
>
> — *Luke 18:27*

✤ Tunasubiri kurudi kwa Bwana Yesu Kristo kunyakua bibi arusi wake. Kisha swali linajitokeza tunawezaje kuelewa jinsi itakavyokuwa. Mara moja tunafikia kikomo cha ufahamu wetu na kisha tunasema, "Ni vigumu kuvuta taswira" (sipati picha) kwa binadamu hili haliwezekani; kulielewa, bali kwa Mungu linawezekana. Lakini hii ni mifano michache niliyowapatia, lakini nina imani mnaelewa nini maana yake. Tunafikia ukomo wa kibinadamu haraka sana, hususani linapokuwa ni jambo la kiroho. Walakini iwapo tunautumia ipasavyo uweza wa Mungu tunaweza kujipanua zaidi ya ukomo wa ufahamu wetu kwa sababu kwa Mungu kila jambo linawezekana. Kwa hili nisingependa kutoa maoni kwamba magumu yote yanaweza kuondolewa papo hapo. Ila kama tukimwamini Mungu, tukajiruhusu kuongozwa na Yeye na kutumia ipasavyo uweza wa Mungu ndipo tunapoweza kwenda mbali zaidi ya ukomo wa kibinadamu.



*Mtume Mkuu Wilhelm Leber*





# africa mashariki








Kanisa Jipya la Kimitume Afrika Mashariki limewasha moto katika kutekeleza hatua itakayo hakikisha kwamba makusanyiko yote katika Afrika Mashariki ni endelevu. Hii ina maana kwamba angalau waumini 60 wanahudhuria kila ibada takatifu. Ili kuweza kufanikisha hili, mpango wa mafundisho umeanzishwa ili kutimiza msingi wa mafundisho ya imani ya kanisa Jipya la Kimitume na kisha mafundisho yataendelea kuhusiana na elimu ya uongozi. Katika kukuza ili wakufunzi wawili wamefundishwa kwa kila eneo la Mtume. Hawa baadaye watawafundisha wakufunzi wa kila wilaya ndogo.

**Hatua ya kwanza** (Utambulisho wa Kanisa Jipya la Kimitume) ilifundishwa mwezi Aprili 2012 kwa waalimu (wakufunzi). Kundi lengwa kwa hatua hii ni kwa watumishi na waumini baada ya mafundisho kwa watumishi na waumini wote madhumuni yafuatayo yatatarajiwa.

1. Watumishi na waumini watakuzwa kiimani katika mafundisho ya KJKM;
2. Imani ya Kanisa Jipya la Kimitume itaendelezwa katika makusanyiko yote;
3. Viwango sawa vya maisha ya imani ya kimitume wapya katika kanda zote kwa nyongeza kwa mafundisho yaliyotajwa hapo juu; Kanisa Jipya la Kimitume limetoa msaada kuisaidia Afrika Mashariki, kwa kuwafundisha viongozi walezi wa nafsi (Mitume na Maaskofu). Kundi la kwanza la watumishi 10 lilifundishwa huko Cape Town Afrika Kusini mwezi Juni 2012. Kisha watawafundisha Maaskofu na Mitume wengine. Hii itakuwa ni njia ndefu katika kuendeleza makusanyiko endelevu na hai katika Afrika Mashariki.

**Kipimo cha pili** cha kutambua kusanyiko endelevu ni kwa njia ya uimbaji. Kwaya za kimakusanyiko zinaendelezwa na mpango wa mafundisho kwa waalimu wa kwaya tayari umeanzishwa. Waumini wanahamasishwa kusaidia mpango huu kwa sababu uimbaji ni sumaku inayoweza kuwavutia wageni weng.

**Tatu;** kuhakikisha malezi bora ya nafsi kwa waumini wote kwa muundo wa kiutumishi ambao upo kwenye mpango wa Kanisa Jipya la Kimitume Kimataifa unatekelezwa. Tunashawishika kwamba baada ya utekelezaji wote wa hatua hizo hapo juu, matokeo yafuatayo yataonekana;

1. Ulinganifu wa watumishi/waumini katika kuendesha shughuli za Kanisa;
2. Kukua kwa imani miongoni mwa watumishi na waumini;
3. Ibada tulivu na zenye mpangilio;
4. Kukamilishwa kwa waumini na kuongezeka kwa kiwango cha mahudhurio;
5. Waumini wapya kwenye kusanyiko;
6. Makusanyiko hai
   - Kushiriki kwa waumini wengi zaidi
   - Kungezeka Ushirika
   - Kuboreshwa Kwaya,
   
   Kuongeza idadi ya ibada yaani katikati ya Juma, Ibada za vijana, watoto n.k.;
7. Kuanzisha makusanyiko mapya;
8. Kuongezeka kwa sadaka.


1


2

1. **_Mtume Mkuu na Mitume wa wilaya Shadreck Lubasi na Charles Ndandula, wakati wa tamasha la uwimbaji jijini Dar-es-Salaam._**
2. **_Wanakwaya wakiwa kwenye ibada takatifu jijini Mwanza._**
3. **_Wanakwaya wakiimba uwimbaji maalumu jijini Dar-es-Salaam._**
4. **_Waumini baada ya Ibada Takatifu ya Mtume Mkuu jijini Mbeya._**
5. **_Kwaya ya watoto._**


3


5


4








**_Mtume wa Wilaya Shadreck Lubasi akiwa pamoja na Mitume wote wa Kenya, Maaskofu na watumishi wengine wa Kanisa baada ya Ibada takatifu ya watumishi na wake zao kwenye kusanyiko la South C, Nairobi tarehe 10 Desemba, 2011._**



**_Mtume wa wilaya Shadreck Lubasi na watumishi kwenye kusanyiko la Butengwa huko Uganda. Aliongozana na Mtume Mwesigwa._**




**_Kusanyiko jipya la Kasoka huko Uganda lilifunguliwa tarehe 27 Aprili, 2012._**



**_Mtume Peter Gitonga na watoto kwenye kusanyiko la Kirinyaga baada ya Ibada ya watoto._**



**_Mtume Byoona na waumini baada ya Ibada ya kufunga mwaka 2011 kwenye kusanyiko kuu la Kampala - Uganda._**

# Wanakipaimara Mwaka 2012

***Wapendwa Wana Kipaimara,***

Wakati umewadia: mnakaribia kuchukua majukumu yenu wenyewe juu ya njia ya maisha yenu pamoja na Kristo. Hivi sasa mtajichukulia na kuweka ahadi kwa ajili yenu wenyewe kwayo wazazi wenu waliahidi kwa niaba yenu wakati mlipobatizwa na kuwekewa mikono. Hivi sasa mtakiri imani yenu na kuweka nadhiri yenu ya Kipaimara. Kwa hiyo mtapokea Baraka kwa ajili ya Uthibitisho wenu, ambazo ni kuwaimarisha juu ya njia yenu.

*Andiko la Biblia kwa ajili ya Uthibitisho wenu limeandikwa katika **Mithali 11:27,** ambapo linasema:*

***"Mtume Byoona na waumini baada ya Ibada ya kufunga mwaka 2011 kwenye kusanyiko kuu la Kampala - Uganda.***

Ujumbe huu ni wa kuwaongoza ninyi.

Jambo la muhimu ni kushindania kile ambacho ni chema. Kwa hakika hilo kila mara siyo rahisi. Ijapokuwa Mtume Paulo alikwishaelezea: "Kwa sababu lile nilipendalo, silitendi; bali lile nilichukialo ndilo ninalolitenda …" Hata hivyo, kama kila mara mtafanya juhudi kwa kutenda mambo mema, Bwana atawaimarisha na kusimama upande wenu. Kushindania kwa ajili ya wema ni ufunguo kwa maisha yaliyotimilika yale yaliyo barikiwa na Mungu. Na pia ndani yake inabeba yenyewe ahadi, ambayo Mtume Paulo alielezea katika kifungu kingine: "Lakini utukufu, heshima, na amani kwa kila mmoja ambaye atendae lililo jema… "Kwa utambuzi huu, kama mtabaki watiifu na waaminifu kwa Bwana, hamtakosa juu ya kufikia lengo la imani yenu.

Ninawatakia siku zenye furaha na kubarikiwa wakati wote, na ninawatumia salaam zangu za upendo ninyi, wazazi wenu pamoja na wapendwa.

*Wenu,*
*Mtume Mkuu*
*Wilhelm Leber*



***District Apostle Shadreck Lubasi and Confirmands at Limuru Town Congregation on 8th April 2012, working area of Apostle Joseph Ekhuya.***



***Askofu David Mwaniki akiwa na Makasisi wa wilaya ndogo ya South C na wana kipaimara tarehe 8 Aprili 2012 katika kusanyiko la South C, Nairobi.***

# Wastaafu



| | |
|---|---|
| ALIZALIWA: | 4/4/1945 |
| KUWEKWA WAWKFU: | 15/8/1982 |
| KUSTAAFU: | 14/8/2011 |

## Mtume Mstaafu Zacharias Nzarumbi

alizaliwa tarehe 4 Aprili 1945 huko Karagwe, Tanzania. Baada ya masomo alifanya kazi kama mtoza ushuru na baadaye akajiunga na Chuo cha Theolojia, ambapo alikuwa mchungaji wa Kiluteri mwaka 1975.

Alimwoa dada Melisa Itebuka mwaka 1967. Ndoa yao ilibarikiwa wakiwa na watoto 8. 5 ni hai lakini 3 wametangulia kuzimu.

Na hivyo Agosti 2011 walikuwa na wajukuu 13 Mtume Nzarombi alipokea ushuhuda wa Kanisa Jipya la Kimitume kutoka kwa Askofu Nyasulu (mstaafu) Januari 1982. Alipokelewa kwenye kanisa la Kimitume na Askofu Donald Kratt (mstaafu) tarehe 14 Agosti 1982. Mwaka huo huo akawekwa wakfu kuwa Kuhani.

Mwaka 1983 aliwekwa wakfu kuwa Mwinjilisti na tarehe 3 Desemba 1983 akawekwa wakfu kuwa Mtume. Alitumika kwenye utume kwa miaka 28 mpaka alipostaafu kwenye ibada kuu iliyoongozwa na Mtume Mkuu Wilhelm Leber tarehe 14 Agost 2011 Jijini Mwanza Tanzania.



**Mtume Mstaafu Zacharias Nzarombi na mkewe Melisa baada ya Ibada takatifu Mwanza Tanzania tarehe 14 Agosti, 2011.**



| | |
|---|---|
| ALIZALIWA: | 4/4/1946 |
| KUWEKWA WAWKFU: | 10/9/1988 |
| KUSTAAFU: | 19/2/2012 |

## Mtume Mstaafu John Mbiti

alizaliwa tarehe 04 Aprili, 1946 huko Kikuyu muumini katika wilaya ya Mwingi, Baada ya elimu yake ya msingi alikuwa mfanyabiashara.

Alimwoa dada Lucia Kyendwa na ndoa yao ilibarikiwa wakiwa na watoto 9. Mtume Mbiti alikutana na ushuhuda wa Kanisa Jipya la Kimitume mwaka 1977 na tarehe 8 April, 1977 alibatizwa na kuidhinishwa na Mtume Wilbert Vovak. Siku hiyo alipokea utumishi wa Ushemasi aliwekewa wakfu kuwa Mtume tarehe 10 Septemba, 1988 na Mtume Mkuu Mstaafu Richard Ferh.

Wakati wa utume wake, imani ya Kimitume ilikuwa kwa kasi huko Mwingi. Alitumika katika huduma hii kwa miaka 23, mpaka kustaafu kwake kwenye Ibada Kuu iliyoongozwa na Mtume Mkuu Wilhelm Leber tarehe 17 Februari 2012 huko Mombasa Kenya.



***Mtume mstaafu John Mbiti na mke wake Lucia mara tu baada ya ibada takatifu Jijini Mombasa, Kenya tarehe 19 Februari 2012.***



# Kuwekwa wakfu Mitume na Maaskofu wapya



| | |
|---|---|
| ALIZALIWA: | 10/4/1964 |
| KUWEKWA WAWKFU: | 14/8/2011 |

## Mtume Steven S. Nhende

alizaliwa kwenye familia yenye Imani ya Kiislamu tarehe 10 Aprili, 1964 kwenye kijiji cha Ishinde wilaya ya Nzega, Mkoani Tabora – Tanzania na alikulia kwenye misingi ya Kiislam. Alipokea ushuhuda wa imani ya Kanisa Jipya la Kimitume kutoka kwa kuhani Julius Tangawizi tarehe 05 Agosti, 2084 na akabatizwa siku hiyo hiyo. Alibaki imara kwenye imani ya kimitume na mwaka 1984 aliidhinishwa na Mtume Mathias NZAROMBI kwenye kusanyiko la Ishinde.

Alimwoa Christina Cheyo na ndoa yao ilibarikiwa wakiwa na watoto watano.

Kwa miaka yote alipokea utumishi kama aifuatavyo;

| | |
|---|---|
| 10.10.1985 | Shemasi |
| 20.01.1988 | Kuhani |
| 19.05.1992 | Mwinjilisti |
| 02.09.1994 | winjilisti wa wilaya |
| 27.01.2002 | Askofu |

Wakati wa Ibada Takatifu Jijini Mwanza, Tanzania tarehe 14 Agosti, 2011, aliwekwa wakfu kuwa mtume. Atakuwa akihudumia Dodoma, Tanzania.



| | |
|---|---|
| ALIZALIWA: | 21/4/1962 |
| KUWEKWA WAWKFU: | 14/8/2011 |

## Mtume Yohonah Byoona

alizaliwa tarehe 21 Aprili, 1962, katika familia ya watoto wane. Amekulia kwenye familia inayomwabudu Mungu, aliweza kwenda shule na kuhitimu elimu ya msingi mwaka 1979 na elimu ya sekondari 1983. Mwaka 1985 alijiunga na Chuo cha Ualimu. Alimwoa Evelyn Aliguma mwaka 1986 na ndoa yao kubarikiwa watoto wawili.

Alipokea ushuhuda wa imani ya Kanisa Jipya la Kimitume kutoka kwa Kuhani Fred Eribankya ambaye baadaye mwaka 1995 alimbatiza na kuidhinishwa na Mtume Edward Seruuma 1996.

Wakati wa Ibada kuu Jijini Mwanza, Tanzania tarehe 14 Agosti, 2011, aliwekwa wakfu kuwa Mtume. Atakuwa akifanya kazi Jijini Kampala, Uganda.

habari za afrika ya mashariki

## Kuwekwa wakfu Mitume na Maaskofu wapya



**ALIZALIWA:** 23/9/1971
**KUWEKWA WAKFU:** 14/8/2011

### Askofu James Ssali

alizaliwa tarehe 23, Septemba, 1971 huko Kitabyama wilayani Masaka, katika familia ya watoto wane. Alisoma katika shule ya Msingi Lutti na kidato cha nne katika shule kuu ya Upili ya Sseke.

Alikaribishwa kwenye Kanisa Jipya la Kimitume yeye pamoja na familia yake na Kuhani Paulo Kawesi, baada ya kuhudhuria Ibada takatifu mara kadhaa wakaamua kubatizwa mwaka 1992 na Kuhani Jonathan Mivule na kuidhinishwa mwaka mmoja baadaye na Mtume Edward Seruuma.

Mwaka 1991 alimwoa Mauricia Nakalema, wamebarikiwa kuwa na watoto wanane. Kwa miaka yote amepitia ngazi za utumishi zifuatazo:-

| | |
|---|---|
| 1993 | Shemasi |
| 1994 | Kuhani |
| 2001 | Mwinjilisti |
| 19.11.2002 | Mchungaji |
| 22.08.2004 | Mwinjilisti wa wilaya |
| 18.04.2010 | Mzee wa Wilaya |

Kwenye ibada kuu ya jijini Mwanza, Tanzania tarehe 04 Agosti, 2011, aliwekwa wakfu kuwa Askofu.

Askofu atakuwa akihudumia pamoja na Mtume Richard Kavuma Magharibi mwa Uganda.



**ALIZALIWA:** 3/5/1960
**KUWEKWA WAKFU:** 14/8/2011

### Askofu James Masila

alizaliwa tarehe 03 Mei, 1960, akiwa mzaliwa wa kwanza kwenye familia ya watoto sita kwenye kijiji cha Kyawango, eneo la Syathani, Machakos. Alijiunga na shule ya msingi mwaka 1970 na kisha akahitimu na kujiunga na shule ya Sekondari Gititu.

Amefanya kazi kwenye sekta binafsi na za umma kabla ya kuwa Bwana shamba Msaidizi. Alimwoa Victoria Ndinda tarehe 03 Machi 1984 na wamebarikiwa kupata watoto watatu. Alijiunga na Kanisa Jipya la Kimitume kupitia kwa Kuhani Dominic Wambua mwaka 1990 ambaye kwa sasa ni Mzee wa Wilaya. Mtumishi huyo huyo alimbatiza yeye na familia yake tarehe 09 Mei, 1992. Baadaye aliidhinishwa na Mtume Patrick Mutara tarehe 20 Mei 1992. Kwa miaka yote amepitia ngazi zifuatazo.

| | |
|---|---|
| 14.11.1993 | Kuhani |
| 18.03.1998 | Mwinjilisti |
| 15.04.2000 | Mwinjilisti wa Wilaya |
| 26.11.2006 | Mzee wa Wilaya |

Kwenye ibada kuu Jijini Mwanza Tanzania tarehe 14 Agosti 2011, aliwekwa wakfu kuwa Askofu. Atatumika pamoja na Mtume Peter Mutisya huko Kenya ya Kati.



**ALIZALIWA:** 1/4/1966
**KUWEKWA WAKFU:** 14/8/2011

### Askofu Fredrick Karyebu

alizaliwa tarehe 01, Aprili, 1966 Kapchorwa wilayani Kamokoli, katika familia yenye watoto wanne. Alisoma katika shule ya msingi Kaserom na kidato cha nne shule ya Sekondari ya Sebel na Kaserem.

Alikaribishwa kwenye Kanisa Jipya la Kimitume na Kuhani Henry Mongo huko Kapchorwa tarehe 8 Novemba, 1992. Kuhani alimwalika kwenye kusanyiko la Yembe ambapo Mtume Francia Kamunyu alipanga kufanya Ibada takatifu. Siku iliyofuata alishuhudiwa na ndugu wanne kutoka kijijini kwao na kwa pamoja wakaanzisha makusanyiko mawili, kwa sasa yanajulikana kama Kamogoyon na Mutungyo.

Mapema tarehe 01 Januari 1998 alioa wamebarikiwa kupata watoto wanne. Kwa miaka yote amepitia katika ngazi zifuatazo.

| | |
|---|---|
| 1993 | Shemasi na Kuhani |
| 24.12.2002 | Mwinjilisti wa Wilaya |
| 11.01.2006 | Mzee wa Wilaya |

Kwenye Ibada kuu jijini Mwanza Tanzania tarehe 14 Agosti, 2011 aliwekwa wakfu kuwa Askofu. Atakuwa akitumika na Mtume Pius Bitayi Mashariki mwa Uganda.



**ALIZALIWA:** 22/3/1968
**KUWEKWA WAKFU:** 14/8/2011

### Askofu Leonard Leopord

alizaliwa kijiji cha Kitwe wilayani Mabira, Mkoani Kagera, Tanzania tarehe 22 Machi, 1968 katika familia ya watoto wanane.

Alipata elimu yake ya msingi katika shule ya Msingi Kitwe mwaka 1977. Alijiunga na Kanisa Jipya la Kimitume akitokea Kanisa la Katoliki la Roma. Alishuhudiwa imani ya Kanisa Jipya la Kimitume na kaka muumini Bazara Bweme kutoka kusanyiko la Kanyamwaha huko Mabira. Alibatizwa na kuhani Karugendo tarehe 02 Februari, 1984 katika kusanyiko la Ibamba na baadaye aliidhinishwa.

Amemuoa Kadogo Agripina na wamebarikiwa kupata watoto wanane. Kwa miaka yote amepitia ngazi zifuatazo:

| | |
|---|---|
| 07.06.1985 | Shemasi |
| 06.07.1988 | Kuhani |
| 02.05.1992 | Mwinjilisti wa Wilaya |
| 22.06.2000 | Mzee wa Wilaya |

Kwenye ibada kuu jijini Mwanza, Tanzania tarehe 14 Agosti, 2011, aliwekwa wakfu kuwa Askofu; Askofu atakuwa akitumika pamoja na Mtume Celestine huko Karagwe, Tanzania.



**ALIZALIWA:** 1/4/1966
**KUWEKWA WAKFU:** 19/2/2012

### Mtume David Nyamai

alizaliwa tarehe 04 Machi, 1964 huko Zombe, Kitui jimbo la Mashariki. Alizaliwa na wazazi wacha Mungu ambao hawakuwa wana wa kimitume.

Baada ya masomo alipata kuwa mwalimu kwa muda mfupi mwaka 1987 kabla ya kujiunga na kozi ya Uhasibu ambayo alifanyia kazi kwenye shirika la Posta na Mawasiliano la Kenya kama afisa wa posta. Baadaye alijiunga na Benki ya Posta ambapo alipanda cheo kutoka Mtunza Fedha na kuwa Meneja wa Tawi mwaka 2001.

Alikuwa mwana mitume mwaka 1988, alibatizwa na kuidhinishwa Machi 1989. Alimwoa Vivi Keneene na ndoa yao imebarikiwa na watoto wane.

Kwa miaka yote amepitia ngazi zifuatazo;

| | |
|---|---|
| Kuhani | 26.07.1992 |
| Kasisi | 07.02.1993 |
| Kasisi wa Wilaya | 20.03.1994 |
| Mwinjilisti | 28.09.1992 |
| Mwinjilisti wa Wilaya | 05.10.2001 |
| Askofu | 11.04.2004 |

Aliwekwa wakfu kuwa Mtume kwenye ibada kuu iliyoongozwa na Mtume Mkuu Leber jijini Mombasa, Kenya tarehe 19 Februari 2012. Mtume atakabidhiwa sehemu ya eneo la Mtume Mstaafu John Mbiti, Kitui, Mwingi na Kamuwongo jimbo la Mashariki.



**ALIZALIWA:** 25/5/1975
**KUWEKWA WAKFU:** 19/2/2012

### Askofu Joseph Musyoki

alizaliwa tarehe 25 Mei, 1975 huko Kavisumi, Kitui jimbo la Mashariki, Kenya. Alijiunga na Kanisa Jipya la Kimitume tarehe 12 Desemba, 1989.

Alifanya kazi kwenye taasisi mbali mbali kabla ya kuwa Meneja wa shamba mwaka 2004 ambapo alifanya kazi mpaka alipoacha kazi na kujiingiza kwenye biashara mwaka 2009. Alipokea ushuhuda wa Kanisa Jipya la Kimitume mwaka 1989 na aliidhinishwa mwaka 1991. Alimwoa Gladys Wayua na wamebarikiwa kupata watoto watatu.

Kwa miaka yote amepitia ngazi za utumishi kama ifuatavyo;

| | |
|---|---|
| Kuhani | 18.07.1993 |
| Mwinjilisti | 13.12.2003 |
| Mwinjilisti wa Wilaya | 16.08.2004 |
| Mzee wa Wilaya | 13.11.2005 |

Aliwekwa wakfu katika utumishi wa askofu kwenye ibada kuu ya Mombasa, Kenya na Mtume wetu Mkuu Leber tarehe 19 Februari, 2012. Askofu atakuwa akihudumia pamoja na Mtume Daudi Nyamai huko Kitui

# picha sanaa



*Mtume Mkuu akipanda ndege uwanja wa ndege wa Mwanza kuelekezea Zurich kupitia Nairobi, baada ya kuitembelea Tanzania.*



*Mtume wa wilaya Shadreck Lubasi, Mtume Mwesigwa na baadhi ya watumishi wa Kanisa kwenye chumba cha maombi kabla ya kuanza kwa ibada takatifu huko Uganda.*



*Wana kwaya wa Dar es Salaam wakiimba nyimbo kwa furaha kwenye tamasha la uwimbaji.*



*Askofu Ngugi akiwasilisha msaada wa Mablanketi kwa wazee na akina bibi huko Embu.*



*Kwaya ikiimba sokoni Ithaga jimbo la kati Kenya – eneo la Mtume Petro Mutisya.*



*Mtume Kavuma akisafiri kwa ngalawa akiwa na baadhi ya watumishi kwenda kuongoza ibada takatifu Kisiwani, Uganda.*


Published by : New Apostolic Church East Africa,
Editorial : District Apostle S. M. Lubasi,
Editor : Publication Committee East Africa,
Layout and design: New Apostolic Work Group Africa.



Administration office, Postal address Box 59041 - 00200, City Square Nairobi,Kenya, East Africa,
Telephone: +254 (20) 6007701 / 6007702 / 6007706, Fax: +254 (20) 6000918, E-mail: admin@nac-ea.org